**TAARIFA YA MHE. HAMZA S. JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU KIKAO KAZI CHA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA WAKURUGENZI WA DIVISHENI/IDARA NA WAKUU WA VITENGO VYA HUDUMA ZA SHERIA SERIKALINI ILIYOTOLEWA KATIKA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MJI WA SERIKALI-MTUMBA TAREHE 05 DISEMBA, 2024**

**Ndugu wanahabari.,**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipo kwa mujibu wa Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018. Serikali kwa makusudi ilifanya mabadiliko na maboresho katika Ofisi yangu kwa lengo la kuboresha na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yaliyoelezwa na kubainishwa katika ibara hiyo.

Mabadiliko haya ndiyo yaliyopelekea kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuimarisha na kuongeza uwezo wa taasisi hizo katika kutoa huduma za kisheria kwa wananchi sambamba na kuiwakilisha Serikali katika mashauri yote ya Madai, Katiba, Haki za Binadamu na Jinai ambayo Serikali kupitia taasisi, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali au Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahusika moja kwa moja au zina maslahi.

Aidha, utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unasimamiwa na kuongozwa na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268, Kifungu cha 8(a). Kwa muktadha huo, Ofisi yangu ina wajibu wa kuratibu na kuishauri Serikali katika masuala yote yanayohusu sheria ikiwemo uandishi wa sheria, upekuzi wa mikataba na makubaliano ya kimataifa.

Hata hivyo, utekelezaji wa majukumu hayo hufanywa na taasisi au watu niliowakasimu majukumu hayo. Kimsingi, majukumu ya Ofisi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yamekasimiwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali waliopo katika Wizara, Taasisi, Wakala za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria kwa niaba yangu.

**Ndugu wanahabari,**
Ili kuzikumbusha Wizara, Taasisi, Idara, Vitengo pamoja na Mawakili wa Serikali wanaotekeleza majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nimeona ni muhimu kuandaa kikao kazi ambacho kitafanyika kesho **tarehe 6 Disemba, 2024 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, uliopo Mji wa Serikali, Mtumba.** Lengo la kikao kazi hicho ni kujadili masuala mbalimbali ya kiutendaji katika utoaji huduma za sheria Serikalini.

Kupitia kikao hicho, pamoja na mambo mengine, tutakumbushana umuhimu wa kuzingatia sheria, taratibu, mipango ya maendeleo, dira na miongozo mbalimbali ya Serikali tunayopaswa kuizingatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku. Mgeni rasmi katika kikao kazi hicho atakuwa **Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.),Waziri wa Katiba na Sheria.**

Hivyo,Pamoja na mambo mengine, katika kikao kazi hicho tutajikita zaidi kujadili masuala yafuatayo;

a) Taarifa za utekelezaji wa kazi za Mawakili wa Serikali;
b) Ushirikiano na umoja baina ya Mawakili wa Serikali;
c) Changamoto za Mawakili wa Serikali;
d) Maadili kwa Mawakili wa Serikali;
e) Utekelezaji wa Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na
**f)** Umuhimu wa ushirikishwaji wa Mawakili wa Serikali katika mambo yanayohitaji ushauri wa kisheria.

**Ndugu wanahabari.,**

Ni matarajio yangu kwamba kikao hicho kitazaa matunda mema kwani naamini kitatoa uelekeo na mikakati ya kutoa hiduma biora za sheria serikalini. Kwani Mawakili wa Serikali ni Jeshi ambalo linalinda uchumi wa nchi kwa kutumia kalamu. Aidha, naamini maelekezo ya Serikali nitakayoyatoa kupitia Kikao hicho muhimu yatatekelezwa ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

**MWISHO**

Nitumie fursa hii kupitia ninyi wanahabari kuwakaribisha Wakurugenzi wa Divisheni/Idara na Wakuu wa Vitengo vya Sheria Serikalini kufika kwa wingi katika kikao hicho bila kukosa ambapo pamoja na mambo mengine, nitatoa maono yangu (Vision) kwenye Sekta ya Sheria nchini